

## Je! Ninahitaji kulipa kiasi gani kupata Kitambulisho cha Taifa?



Kitambulisho cha Taifa hutolewa bure kwa mara ya kwanza lakini ada ya Shs 50000/= za Uganda inatozwa kulipia kitambulisho kilichopotea, kilichoharibika au kilichofifia.

## Nimesajili na sijawahi kupata Kitambulisho cha Taifa.

- Usajili na utoaji wa vitambulisho vya Taifa unaendelea katika wilaya zote za Uganda na katika ofisi tano za KCCA, Kampala.
- Piga \*216# kuangalia taarifa ifuatayo;
  - i. Mahitaji ya Maombi
  - ii. Viwango vya maombi
  - iii. Badilisha Kitambulisho
  - iv. Marekebisho ya taarifa ya Kitambulisho
  - v. Angalia NIN

## Ninaweza kujiandikisha wapi nikiwa nje ya Uganda?

[Efforts are under way to establish registration at selected missions and embassies.](#)

## Je! Ninaweza kumtuma mtu kunichukulia Kitambulisho cha Taifa?

Utoaji wa Kitambulisho cha Taifa kupitia wakala unawezekana pale ambapo mwombaji hajaweza kwa sababu zifuatazo; ugonjwa au uzee, walemavu wa mwili, kufungwa jela na watu wanaoishi Ughaibuni

- i. Fomu 8 ya idhini na hati zinazostahili
- ii. Risiti ya Usajili kuhusu maombi haya (Fomu 5)
- iii. Uthibitisho wa Mtu kutokuwa na uwezo wa kupokea Kitambulisho
- iv. Kitambulisho cha Taifa cha wakala

## Je! Ni lini mtu anaweza kubadilisha Kitambulisho cha Taifa?

Mtu akipoteza Kitambulisho cha Taifa, anahitaji kuripoti kwa polisi, kufanya malipo ya shilingi za Uganda, 50,000/= katika benki utakayopendelea.

Unahitaji kujaza fomu ambayo unaweza kupakua mtandaoni, kutoka kwa wavuti ya NIRA [www.nira.go.ug](http://www.nira.go.ug), au zipate bila malipo kutoka ofisi yetu yoyote nchini na mchakato wa kubadilisha kitambulisho utaanza.

Kama kuna haja ya kubadilisha taarifa kwenye Kitambulisho cha Taifa: zinaweza kuhusisha kubadilisha jina, eneo, mabadiliko ya jinsia na vingine.

## Je! Ninahitaji nini kubadilisha taarifa kwenye Kitambulisho cha Taifa?

Hii inawezekana tu kama una hati au nyaraka zifuatazo;

1. Hati ya kubadilisha jina
2. Tamko la Kisheria
3. Vyeti vya ndoa
4. Vyeti vya shule
5. Vyeti vya talaka
6. Risiti za malipo
7. Vyeti vya kuzaliwa na vingine vyote kama vitakavyohitajika.

### NIRA (MAKAO MAKUU)

Kiwanja cha Uhuru cha Taifa, Kololo Airstrip  
S.L.P 26529, Kampala-Uganda  
Simu (Mapokezi): +256 312119600

### Kwa Maulizo ya Wateja, wasiliana na:

0800211700 (Kituo cha Simu)

### Kwa Maulizo juu ya Mahusiano ya Umma,

Simu: +256 312119605

Nira\_Ug NIRA [nira.go.ug](http://nira.go.ug)



# JINSI YA KUJIANDIKISHA KUPATA KITAMBULISHO CHA TAIFA



Mamlaka ya Usajili na Utambulisho wa Taifa (NIRA) ilianzishwa na Sheria ya Usajili wa watu ya 2015.

## Mamlaka ina majukumu yafuatayo;



Kusajili Raia na kuawapa Nambari ya Utambulisho ya Kitaifa (NIN) na vitambulisho vya Taifa



Kusajili wanaozaliwa wote, vifo na Amri ya Kuasili na kutoa hati zinazohitajika



Kuunda, kusimamia na kudumisha Daftari la Utambulisho la Taifa

**Taarifa hiyo katika Daftari la Utambulisho la Taifa inapatikana na inaweza kutumiwa na vyombo vya serikali, vyombo vya kibinafsi na watu binafsi.**

Kipeperushi hiki kinatoa mwongozo wa haraka wa kuelewa mchakato wa usajili wa vitambulisho vya kitaifa, vizazi, vifo na Amri ya kuasili mtoto.

## Nani anapaswa kusajiliwa?

- Raia wote wa Uganda.
- Wageni wote wanaoishi kihalali nchini Uganda watasajiliwa.



## Usajili unafanyika wapi?

- Usajili na utoaji wa vitambulisho vya Taifa unaendelea katika wilaya zote za Uganda na katika ofisi tano za KCCA, Kampala

## A. MAHITAJI YA RAIA KUJISAJILI KWA VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA KUZALIWA

1. Barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa (LC1) iliyopigwa mhuri na DISO ikielezea majina ya wazazi wa mwombaji, kabila na ukoo.
2. Picha za wazazi, vitambulisho vya taifa ikiwa wako hai, ikiwa wamekufa, barua ya maelezo inapaswa kuonyesha wazi hivyo.
3. Hati nyingine yoyote kama cheti cha kuzaliwa

## B. MAHITAJI YA RAIA KUJISAJILI KWA VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA KUANDIKISHWA

1. Mahitaji yote katika “A” hapo juu.
2. Nakala ya cheti cha uraia kwa kurithi au uraia kwa kujiandikisha kama inavyofaa.
3. Nyaraka nyingine zozote n.k. nakala ya cheti cha kuzaliwa, pasipoti, cheti cha Ndoa, hati za kitaaluma, hati ya kuendesha gari, cheti cha Ubatizo, kadi ya wapiga kura nk.
4. Nakala ya Vitambulisho vya Taifa vya wazazi (kama inapatikana).

## C. RMAHITAJI YA RAIA KUJISAJILI KWA VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA URAIA WA NCHI MBILI

1. Nakala ya Cheti cha uraia wa nchi mbili kilichotolewa na DCIC
2. Pasipoti (za) ya mwombaji
3. Nakala ya NID ya wazazi (kama inapatikana)